



Australian Government  
AUSTRAC

FIGHTING  
FINANCIAL  
CRIME  
TOGETHER

# Maagizo ya Uhamisho wa Fedha za Kimataifa (IFTI)

## Taarifa muhimu kwa watoa huduma za kifedha

### IFTI ni nini?

IFTI ni maagizo ya kuhamisha pesa au mali:

- kutoka Australia kwenda nchi nyingine **au**
- kuingia Australia kutoka nchi nyingine.

Mteja wako anaweza kuwa mtumaji au mpokeaji katika muamala.

### Ni wakati gani nataka kuwa kuripoti IFTI?

Unapopokea maagizo ya kutuma au kupokea fedha au mali ndani au nje ya Australia, lazima uwasilishe ripoti ya IFTI kwa AUSTRAC.

Ripoti za IFTI lazima ziwasilishwe ndani ya siku **10 za biashara**.

Ikiwa utakusanya pesa pamoja kutoka kwa wateja kadhaa ambao wanatumia fedha kwenda sehemu sawa, lazima uripoti maagizo ya kila mteja katika ripoti tofauti ya IFTI.

### Kwa nini ni muhimu kuripoti IFTIs?

AUSTRAC na washirika wetu hutumia habari tunazopokea katika IFTIs pamoja na habari tunazopokea katika ripoti zingine kusaidia kupambana na ugaidi, wahamiaji haramu, biashara ya dawa za kulevya, utakatishaji fedha, ukwepaji wa kodi na uhalifu mwingine mkubwa.

Ripoti yako inaweza kuwa ufunguo wa uchunguzi au inaweza kusaidia kukomesha shughuli za jinai - kwa hivyo ni muhimu kuripoti IFTIs zote.

Kumbuka kwamba IFTIs zina taarifa binafsi za wateja wako ambazo zinapaswa kulindwa.

### Usahihi wa IFTIs

Usahihi wa IFTIs zako kutaokoa muda wako na kuhakikisha AUSTRAC inapokea habari muhimu ambayo inaweza kusaidia kuzuia shughuli za jinai.

Ili kukusaidia kuandaa vizuri, **angalia kwa uangalifu kwamba maelezo yafuatayo yamejumuishwa na sahihisha** wakati wa kuwasilisha IFTI zako:

- Mteja anaegiza na mteja mnufaika ikiwa ni pamoja na majina yao kamili ya kisheria - sio herufi za kwanza au vifupisho. Jumuisa majina mengine yoyote ikiwa yanajulikana
- Maelezo ya kitambulisho cha mteja kama vile aina ya kitambulisho na nambari ya kitambulisho
- Maelezo ya anwani. Lazima ujumuishe anwani ya mahali, masanduku ya posta hayawezi kutumika
- Maelezo ya uhamisho kama tarehe ya uhamisho, aina ya fedha, mwelekeo wa uhamisho na kumbukumbu namba ya muamala, ikiwa inatumika
- Hakikisha haujaacha sehemu yoyote wazi ikiwa taarifa inapatikana.

Tunakuhimiza pia ujumuishe habari ya ziada kama anwani ya itifaki ya wavuti (IP) au kitambulisho cha kifaa cha wateja wa mtandaoni.



AUSTRAC au wakala mshirika pia anaweza kukutumia notisi ya maandishi ikihitaji habari zaidi kuhusu ripoti ya IFTI. Kwa orodha ya washirika wa serikali tazama [austrac.gov.au/government-partners](http://austrac.gov.au/government-partners).

AUSTRAC au wakala mshirika pia anaweza kukutumia notisi ya maandishi ikihitaji habari zaidi kuhusu ripoti ya IFTI. Kwa orodha ya washirika wa serikali tazama

## Ninawasilishaje ripoti ya IFTI?

Unawasilisha ripoti za IFTI kupitia akaunti yako ya AUSTRAC ya mtandaoni. Unaweza kufikia akaunti yako kupitia tovuti ya AUSTRAC.

## Ni nini matokeo ya kutowasilisha ripoti za IFTI?

Ikiwa unashindwa kuripoti IFTIs au kutimiza majukumu yako mengine, AUSTRAC inaweza kuchukua hatua ikiwa ni pamoja na kutafuta adhabu.

AUSTRAC pia inaweza kukataa, kughairi au kusitisha usajili wa watoaji wa huduma ya pesa ikiwa wana hatari ya kuwezesha utakatishaji pesa, ufadhili wa ugaidi, au uhalifu mwingine mbaya.

Ni kinyume cha sheria kutoa huduma za kuhamisha pesa ikiwa tutakataa, kughairi au kusimamisha usajili wako.

Hakikisha biashara yako ina mifumo tayari ili kuzingatia majukumu yote ya kuripoti ya IFTI. Pitia michakato yako ya biashara mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa shughuli zote zinaripotiwa kwa usahihi na kwa wakati.

## Je! Muamala unajumuisha majukumu mengine ya kuripoti?

### Kizingiti cha miamala

Ikiwa muamala wa mteja unahusisha fedha taslimu AUD 10,000 au zaidi au thamani sawa katika fedha za kigeni, lazima pia uwasilishe ripoti ya kizingiti cha miamala (TTR) kwa AUSTRAC.

Hii inatumika tu kwa pesa taslimu (noti na sarafu). Huna haja ya kuripoti TTR ikiwa mteja anaweka pesa kwenye akaunti yako ya benki au ikiwa mteja anatuma pesa kwako kwa kutumia uhamisho wa benki.

### Maswala ya kutiliwa shaka

Ikiwa una sababu nzuri za kushuku kuwa mtu au muamala unahusishwa na uhalifu au sio anaejitambulisha kuwa, lazima pia uwasilishe ripoti ya jambo linaloshukiwa (SMR) kwa AUSTRAC

Kwa habari zaidi juu ya hizi na majukumu mengine ya kuripoti, tembelea [austrac.gov.au/reporting](http://austrac.gov.au/reporting).

